

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dar es Salaam
29 Januari, 2026

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA AZINDUA MKAKATI WA KITAIFA WA KISAYANSI WA KKK

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amezindua rasmi Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa Elimu ya Awali na wanafunzi wa Darasa la I na II, jijini Dar es Salaam.

Mkakati huo ni miongoni mwa ahadi za siku 100 zilizotolewa na Rais Dkt. Samia wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2025, na ni msingi wa ujifunzaji unaolenga kuhakikisha watoto wote wanamudu stadi za msingi za kusoma, kuandika na kuhesabu mapema kabla ya kufika Darasa la Tatu, ili kuwawezesha kujifunza kwa ufanisi katika hatua zinazofuata za elimu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Rais Dkt. Samia amesema kuwa KKK ni msingi wa ujifunzaji wote, akisisitiza kuwa mtoto anayekosa msingi huo hubaki nyuma kielimu na hupata ugumu wa kumudu masomo ya juu zaidi.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa maandalizi thabiti ya Mkakati huu, akieleza kuvutiwa na matumizi ya mbinu shirikishi za ujifunzaji zilizooneshwa wakati wa uzinduzi kwa kutumia zana na nyenzo bunifu zinazopatikana nchini.

Rais Dkt. Samia amelekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na wizara za kisekta zinazohusika na maendeleo ya awali ya mtoto, ili kuhakikisha Mkakati huu unatekelezwa kikamilifu katika ngazi zote.



[Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano /
ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania /
ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania](#)



Katika utekelezaji wa Mpango Mkakati huo, Rais Dkt. Samia ameagiza kufanyika kwa tathmini za mapema na endelevu za ujifunzaji ili kubaini changamoto kwa wakati kwa kuzingatia matokeo halisi ya watoto, badala ya taarifa pekee.

Katika kufanikisha hilo, amesisitiza umuhimu wa kuwawezesha walimu kwa mbinu za kisasa na nyenzo za kufundishia, pamoja na kuimarishwa kwa ukaguzi wa elimu na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji, ili kubaini changamoto kwa wakati na kuchukua hatua stahiki.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Samia ameeleza Mkakati wa KKK kuwa sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023), pamoja na mchango wa Tanzania katika kutekeleza Ajenda ya Afrika 2063 na Lengo namba Nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 4) kuhusu Elimu Bora.

Halikadhalika, Rais Dkt. Samia ametambua mchango wa sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika utoaji wa elimu nchini, na kusisitiza umuhimu wa ushiriki wao katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati huo.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema Serikali imetekeleza ahadi ya Rais kabla ya kuisha siku 100 za malengo ya utekelezaji, na kuongeza kuwa Mkakati wa KKK utatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano hadi mwaka 2030/2031, huku tathmini ya utekelezaji ikitolewa kila mwaka.

TAARIFA KWA MHARIRI:

Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa Elimu ya Awali na wanafunzi wa Darasa la I na II, ni mkakati wa kitaifa unaolenga kubadili matokeo ya ujifunzaji wa awali kwa kuhakikisha watoto wanamudu kusoma, kuandika na kuhesabu mapema, kupitia mbinu zinazopimika na uwajibikaji wa wazi wa utekelezaji.

Utekelezaji wa Mkakati huu unaenda sambamba na maboresho ya miundombinu na rasilimali watu yaliyofanywa katika Sekta ya Elimu, kama vile ujenzi wa madarasa ya elimu msingi kutoka **151,315** mwaka 2021 hadi **184,850** mwaka 2025, pamoja na mpango wa ajira **7,000** za walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati, ambapo tayari walimu **6,044** wamekwishaajiriwa.



Shaaban Kissu

K.n.y. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu